



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA JIJI LA TANGA



Kumb Na. TCC/S.20/12/C/58

Tarehe: 17/04/2023

TANGAZO LA KAZI

Halmashauri ya Jiji la Tanga imepokea kibali cha ajira Mpya kutoka ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma chenye kumb Na. FA.97/228/01 "TEMP"/06 cha tarehe 06 April, 2023

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Tanga anapenda kuwatangazia nafasi za kazi kwa watazania wenye sifa waweze kuomba kama ifuatavyo:-

1. Mtendaji wa Mtaa Daraja III Mshahara TGS B: Nafasi 10

Sifa za kuajiriwa:-

Waombaji wawe na Elimu ya kidato cha IV/VI waliohitimu Astashahada (NTA Level 5) katika fani ya Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii (Sociology), Usimamizi wa Fedha (Finance Management), Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo Dodoma au chuo chochote kinachotambuliwa na serikali.

Kazi na majukumu:


- i. Mtendaji Mkuu wa Mtaa
- ii. Mratibu na msimamizi wa upangaji wa mipango shirikishi ya maendeleo ya Mtaa.
- iii. Mshauri wa Kamati ya Mtaa kuhusu Mipango ya Maendeleo katika Mtaa;
- iv. Msimamizi wa utekelezaji wa Sheria ndogo pamoja na sheria nyingine zinazotumika katika Mtaa.
- v. Mshauri wa Kamati ya Mtaa kuhusu masuala ya Ulinzi na Usalama;
- vi. Msimamizi wa utekelezaji wa mikakati mbalimbali inayohusu uondoaji wa njaa na umaskini katika mtaa;
- vii. Kusimamia ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri na kutunza kumbukumbu za walipa kodi wote;
- viii. Kuandaa na kutunza rejesta ya wakazi wote wa Mtaa na;
- ix. Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata

MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIWA KWA WAOMBAJI WOTE:

1. Muombaji awe Raia wa Tanzania mwenye umri wa miaka 18 hadi 45
2. Maombi yaambatanishwe na vivuli vya vyeti, picha moja ya paspoti saizi iliyopigwa hivi karibuni, maelezo binafsi (CV) ya muombaji na namba ya simu.
3. Waombaji wawe na Kitambulisho cha NIDA au namba ya NIDA
4. Waombaji wenye vyeti vya kidato cha nne na taaluma ambavyo vimepatikana nje ya Nchi wahakikishe vimehakikiwa na Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA). Na Baraza la Elimu ya Ufundi (NACTE).
5. Waombaji waliofukuzwa kazi, kupunguzwa kazi au kuachichwa kazi katika utumishi wa Umma hawaruhusiwi.
6. Waombaji ambao hawana sifa wanashauriwa kutokuomba kwa sababu barua zao hazitashughulikiwa
7. Watumishi waliowahi kuajiriwa Serikalini na kupata Cheki Namba hawataajiriwa tena bali wataajiriwa baada ya kupata kibali cha Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.
8. Juu ya bahasha aandike kazi aliyoomba,
9. Transcript na provision result havipokelewi
10. Maombi yote yatumwe kwa:-

Mkurugenzi wa Jiji,
09 Barabara ya Hassan Ngwilizi,
21101 Centra Tanga,
S.L.P. 178,
TANGA

11. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 30/04/2023 saa 9.30 mchana.


Dkt. Sipora J. Liana
MKURUGENZI WA JIJI
MKURUGENZI WA JIJI
TANGA

09 Barabara ya Hassani Ngwilizi, 21101 Central Tanga, S.L.P 178 Tanga, Simu: +27 2643068, +27 2644530/3.
Nukushi: +255 27 2644141/272647905. Tovuti: info@tangacc.go.tz. Tovuti: www.tangacc.go.tz